REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Thursday, 2nd September, 2021

The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.

[The Speaker (Hon. Patrick Waigwa) in the Chair]

PRAYERS

QUORUM CALL

Speaker: Clerk, kindly confirm whether we have got quorum.

(Lack of quorum confirmed)

Speaker: Serjeant at Arms to ring the bell for ten minutes or until we achieve quorum.

(The quorum bell was rang for five minutes)

Speaker: Clerk, confirm whether we have got quorum.

(Quorum confirmed)

PAPERS

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS BY THE LABOUR, SOCIAL WELFARE AND COMMUNITY SERVICES COMMITTEE

Hon. Patricia Muthoni: Thank you, Mr. Speaker. I beg to lay the report of the Committee on Labour, Social Welfare and Community Services on County Governmnet of Laikipia County Executive) quarterly report and financial statements for the period ended 31st December, 2019 dated 26th August, 2021.

NOTICE OF MOTION

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS BY THE LABOUR, SOCIAL WELFARE AND COMMUNITY SERVICES COMMITTEE

Hon. Patricia Muthoni: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to give notice of the following motion;

> THAT this Assembly adopts the report of the Committee on Labour, Social Welfare and Community Services on County Governmnet of Laikipia County Executive) quarterly report and financial statements for the period ended 31st December, 2019 dated 26th August, 2021.

STATEMENTS

NOTICE PAPER

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Mr. Speaker. On behalf of the HBC, it is notified that the House Business Committee has approved the following tentative business to appear in the order paper for Tuesday (Afternoon) September 7th, 2021

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

A. **PAPERS**- County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th September, 2019 by the Trade Tourism and Cooperatives Committee.

B. **PAPERS**- County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 31st December, 2019 by the Finance and County Planning Committee.

C. **PAPERS**- Public participation report on the Laikipia County Climate Change Bill, 2021.

D. **NOTICES OF MOTIONS**- County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 30th September, 2019 by the Trade Tourism and Cooperatives Committee.

E. **NOTICES OF MOTIONS**- County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 31st December, 2019 by the Finance and County Planning Committee.

F. **NOTICES OF MOTIONS**- Public participation report on the Laikipia County Climate Change Bill, 2021.

G. **MOTION**- County Government of Laikipia (Executive) quarterly report and financial statements for the period ended 31st December, 2019 by the Labour, Social Welfare and Community Services Committee.

It is notified that the House Business Committee has approved the following tentative business to appear in the Order paper for Wednesday (Morning) September 8th, 2021.

A. **MOTION**- County Government of Laikipia (Executive) quarterly report and financial statements for the period ended 30th September, 2019 by the Trade Tourism and Cooperatives Committee.

It is notified that the House Business Committee has approved the following tentative business to appear in the Order paper for Wednesday (Afternoon) September 8th, 2021

A. **BILL-** Laikipia county youth services bill,2020(Committee of the whole house)

B. **BILL**-Laikipia County youth services bill, 2020(Third Reading)

C. **MOTION**- County Government of Laikipia (Executive) quarterly report and financial statements for the period ended 31st December, 2019 by the Finance and County Planning Committee.

It is notified that the House Business Committee has approved the following tentative business to appear in the Order paper for Thursday (Afternoon) September 9th, 2021

A. **MOTION-** Public participation report on the Laikipia County Climate Change Bill, 2021.

Mr. Speaker, those are the tentative businesses that the committee has approved. I am urging the Chairs of the said committees especially the Chairs of Finance and Trade have to prepare themselves for next week because this House is waiting for those businesses. Thank you.

MOTIONS

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS BY THE AGRICULTURE, ENVIRONMENT AND NATURAL RESOURCES COMMITTEE

(Resumption of a previous debate held on Wednesday, 1st September, 2021 at 2.30 p.m.)

Hon. Simon Kanyutu: Thank you, Mr. Speaker. I beg to move the following motion;

THAT this Assembly adopts the quarterly report and financial statements for the period ended 31st December, 2019 for the department of agriculture, Livestock and Fisheries by Agriculture, Environment and Natural Resources Committee dated 19th August, 2021.

Speaker: If there is no any debate on the motion, the mover can give a reply.

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Mr. Speaker. On behalf of Hon. Mugweru…

Speaker: That one is on behalf of Hon. Simon Kanyutu.

Hon. Stephen Ndiritu: I think Hon. Mugweru was the Mover of that motion.

Speaker: Moving on behalf, okay.

Hon. Stephen Ndiritu: On behalf of Hon. Mugweru who was doing it on behalf of the Chair.

Speaker: You are replying on behalf of the Chair of Agriculture Committee just the way Hon. Mugweru was doing on behalf of the Chair.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Nafikiri huu ni mswada tulioweza kuujadili jana na ulikuwa unaeleza kuhusu idara ya Kilimo na ripoti ya vile ambavyo wametumia hiyo pesa. Maoni yote yaliyotolea na Wajumbe ni maoni ambayo kamati, kwa niaba ya mwenyekiti, tutaangalia na kuzingatia na kuhakikisha kuwa idara imetumia pesa kama ilivyokusudiwa. Nashukuru.

(Question put and agreed to)

MOTION

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS BY THE TRANSPORT AND PUBLIC WORKS COMMITTEE

Hon. Catherine Nyawira: Mr. Speaker, I beg to move the following motion;

THAT this Assembly adopts the report of the Committee of Transport and Public Works on the County Government of Laikipia quarterly report and financial statements for the period ended 31st December, 2019 dated 23rd August, 2021.

Hon. Speaker, on behalf of the Chair and the Members, I want to first thank them for cooperation in putting together this financial document which comes to the Assembly during every quarter and has a lot of tabulations and tables. As a committee, we are mandated to go through it, scrutinize it and try to summarize it for the other Members, and that is what we have to do.

Committee membership

The Chairperson of this committee is Hon. Daniel Mugweru, the Vice-Chair is Hon. Stephen Ndiritu; Hon. Wilson Wakahiu, Hon. Mary Samken and I are members.

Committee mandate

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Speaker, the mandates of the committee range from over sighting the roads and other infrastructural areas. In the financial operations of this department, No. 4.0, the financial operations performance, there is a table there which has the land rates and vehicle parking fees. These are the revenues that the County generated in the year 2019/20 and what they had targeted as well as what they actually realized.

You will realize, for example, that in 2019/20 four million was collected. In quarter two, the department collected four million and seven million in quarter one, which was something that went up. That is not shown in the table but I believe it will show as we proceed. You will also realize that in quarters two and one, there was an increment of about one million on parking fees.

In the year 2019/20, the County had a total budget of Kshs. 178 million for the vote on RMLF. In this second quarter the County received revenue of Kshs.29 million. Hon. Speaker and the House, you will agree with me that RMLF has done a lot of work within the urban centres like Nyahururu, Nanyuki and Rumuruti. The roads that have been done there are quality, well done and well-supervised. I believe this is probably because this is money that comes down from the National Government and is supervised directly by the National Government.

It is probably a challenge to the committee because these roads are the talk of even Nyandarua and Meru Counties. They come here and see that the town has really changed. As a committee, and other committees, I urge that we do work of such quality and allocate enough money to projects so that the project has adequate money to be able to realize proper, quality work.

Committee observations

1. The committee observed that during this 2nd quarter a total amount of Kshs.67 million was paid for road works and at the end of the quarter there was a notable pending bill of Kshs.139 million.

Committee recommendations

1. The committee recommended that the department fast tracks the procurement process for all projects that it intends to be done so as to ensure that the payments can be made timely.

2. The department should ensure that all the projects committed are within the actual budget allocation so as to prevent occurrence of pending bills.

Hon. Speaker, I think time and again when we are passing the budget; I have always emphasized in my contribution that when this House passes a budget on roads, let us have committees be supplied with BQs so that we can be able to know that this road has actually been planned for, the bill of quantities has been done, so that even oversight is easy and the contractor is able to get that job on time.

Before we pass these budgets, I think the BQs are never done, they are done later. By the time people go to IFMIS it is failing, so work takes time and is done in the last two months, and I believe this is one of the causes of pending bills. I beg that this House adopts this committee's report and financial statements for the period ended 31st December, 2019 for the Transport department. I wish to call upon Hon. Stephen Ndiritu to second this report.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Nasimama kuunga mkono ripoti ya Kamati ya Uchukuzi na Kazi za Umma. Nafikiri Mheshimiwa Nyawira ameweza kueleza

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

vizuri sana, na hii ni idara ambayo kwa wakati mwingi imekuwa ikituangusha sana. Nafikiri Wajumbe wameweza kuikagua hii ripoti na kuna mambo mengine tunayoona wamefanya vizuri hasa upande wa malipo ya ardhi.

Tumeweza kuona ya kwamba wameongeza uokotaji wa ushuru kutoka milioni tatu hadi milioni saba na hilo ni jambo la busara na litaweza kusaidia hii kaunti yetu hasa wakati tunahitaji pesa za maendeleo. Ni vizuri pia tuweze kujua ni njia ipi ambayo walitumia kuweza kupata nyongeza ya hizi milioni tatu ambapo hawakuweza kupata robo ya pili. Ukiangalia hiyo tofauti ni kumaanisha ya kwamba kuna ulegevu ama wamesukuma wananchi kwa njia isiyo ya haki na ni vizuri tuwe tunafuatilia mambo kama hayo.

Tunaweza kukaa hapa tukiridhika ilhali wananchi wetu wanaumia. Kama vile tumesomewa ripoti, kamati tuko na jukumu la kuwaita hao washikadao ama viongozi katika hiyo idara ndiyo waweze kufafanua haya maswala kwa sababu yako kwa hii ripoti na yamejitokeza kinagaubaga kwamba kaunti yetu tunasonga mbele. Tunaposonga mbele ni vizuri tujue tunasonga mbele kwa njia ipi.

Bwana Spika, 2019 ni wakati ambapo Korona iliweza kutokea na tunajua ya kwamba huo mwaka kulikuwa na changamoto. Hilo ni jambo ambalo sisi kama kamati tunafuatilia na tutaweza kuhakikisha...

Speaker: There was no Covid-19 in the year 2019 but in 2020.

Hon. Stephen Ndiritu: Bwana Spika, nilidhani Korona inaitwa Covid-19 kwa sababu ilikuja mwaka wa 2019.

Speaker: But in this country, Covid-19 started in the year 2020.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika kwa kuweza kunipatia ripoti ambayo kwa kweli nimekumbuka Korona iliweza kutangazwa Kenya 2020 mwezi wa tatu. Nakubaliana nawe lakini ilikuwa imetokea mwaka wa 2019 kwa nchi kama China na zinginezo. Kuna zile pesa ambazo pia ni za RMLF ambazo ni 178,000,000. Ni pesa ambazo zinafaa kutumika katika marekebisho ya barabara katika mashinani. Nafikiria ya kwamba hizi pesa zinafaa kuwa zinasaidia watu mashinani kama kule kwetu upande wa Sweet Waters, Njoguini, Ruai na Baraka lakini katika hii kaunti yetu tumeweza kuona ya kwamba zinatumika...

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, ningeteka Mheshimiwa anitolee ufafanuzi zaidi kwa sababu Nanyuki na Nyahururu ndio walifaidika zaidi na kwa hivyo anapozitaja hizo fedha, hao ndio wamesaidika zaidi na *Road Maintenance Levy Fund*. Hizo pesa amesema ni za mashinani lakini mimi niko na ushahidi wa kutosha ya kwamba huko kwake karibu sokoni kuna lami, Nanyuki na pia Nyahururu. Kwa hivyo sijui atanifahamisha aje zaidi lakini yeye hata kama anaonekana kama anatutetea akisema Njoguini na kwingine, akiri kwanza ya kwamba asilimia fulani ya kwake ameweza kusaidika sana na hizo lami.

Asije akatudanganya sisi ambao tunatoka mashinani kusema ya kwamba hizi pesa ni za mashinani ilhali yeye yuko na lami. Ningetaka anielezee zaidi kama anajua ni za mashinani aweze kueleza ni barabara ngapi katika maeneo ya uwakilishi kwa sababu tuko na zaidi ya kumi na tano. Nina uhakika ya kwamba ni watu wanne ambao wamefaidika na hizo pesa ambao ni Nanyuki, Nyahururu, Thingithu na Rumuruti. Kwani sisi ni namna gani na sasa ameanza kusema ya kwamba aweke Njoguini na kwingineko. Kwa hivyo tunapokaa hapa, kidogo, asiendelee kuonyesha huko Njoguini ilhali mimi niko na mji wa Matanya na unahitaji lami kama hizo barabara ambazo ziko kwake.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Ndipo tulikuwa tunapigia debe na sioni aibu nikisema ya kwamba tunastahili kuchukua ruzuku kuweza kuinua miji mingine ya kwetu. Mimi niliunga mkono kwa sababu ya hiyo. Mji wangu kama wa Matanya unatoa kodi nyingi katika hii kaunti lakini ukitembea pale wafanyi biashara wanapaka rangi kila baada ya miezi mitatu. Ukiingia kwenye hizo maduka utaona aibu ilhali tunalipa kodi. Kwa hivyo...

Speaker: Hon. Mutahi, you know you rose to seek for clarification but you cannot go ahead and start debating and telling us how Matanya looks like. The Member will clarify...

Hon. Mutahi Muritu: Ni kuniumiza ameanza kuniumiza akisema...

Speaker: Kindly be seated.

Hon. Mutahi Muritu: Thank you.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika kwa kunikinga. Mheshimiwa Mutahi ameweza kujieleza lakini amekuwa kama ni kunisomea kwa sababu ya yale ambayo nilikuwa nimesema. Nilipoanza kuchangia hii ripoti, niliweza kueleza ya kwamba hizi pesa sana sana zinafaa kuingia mashinani na nikaweza kutaja mahali mimi ningetaka. Na kwa hivyo Mheshimiwa Mutahi atakuwa na nafasi, hata yeye atataja Matanya, Muiyogo, Solio na kwingineko.

Bwana Spika, hizi pesa, kwa kweli wale ambao wamefaidika na hizi pesa ni mji wa Nanyuki na Nyahururu na ndio maana wakati tunaongelelea hii ripoti, utaweza kuona ya kwamba wale Wajumbe ambao wanaotoka sehemu hizo hawako hapa kwa sababu wanataka tu tusome, tulalamike bila wao kusikia. Kwa hivyo hili ni jambo ambalo tutalitilia maanani.

Ningetaka kufafanulia Mheshimiwa Mutahi ya kwamba zile pesa ambazo zimepelekwa Thingithu ni kama tone kwa ile wodi. Zile barabara ambazo zimeweza kujengwa huko ni barabara ambazo hazijafikisha kilomita moja. Kwa hivyo ningeomba Mheshimiwa Mutahi aweze kunionea huruma. Niweze kumfafanulia pia ya kwamba hata yeye ni anafaidika na MRF ambayo ni *rural maintenance* na naweza kutoa mfano kwa sababu mimi ni shahidi ya kwamba amejengewa barabara kutoka Thome mpaka Muiyogo na hii pesa. Bwana Spika

Bwana Spika, naona hata yeye aliweza kutuchenga na ndio maana nateta ili nipate pesa kama hizi Ruai, Baraka na kwingineko. Kwa hivyo wakati tunasema tutumie hizi pesa vizuri, ni vizuri wakati tunafanya bajeti mimi pamoja na Mheshimiwa Mutahi, Mheshimiwa Lochimidi na wale wengine tuungane ili hizi pesa zipelekwe wodi zingine ambazo hazikuweza kupata pesa za Rural Maintenance.

Sijui kama Miji ya Nanyuki na Nyahururu ni *Rural* na ningependa kufahamishwa. Huku ndiko hizi pesa zimeongezwa. Wananchi wengine wa Laikipia wananyimwa haki na nafasi ya kupata hizi pesa ili ziwasaidie. Jambo lingine ambalo limeweza kujitokeza katika hii ripoti ni ya kwamba wakati tunapeana kazi ya kujenga barabara na kazi zingine kutoka Idara ya Miundombinu. Naungana na Mheshimiwa Nyawira kwamba wakati tunatengeneza bajeti kabla ya kutengeneza bajeti ni lazima tuzingatie BQ.

Bwana Spika, mara mingi tunafanya bajeti na inapita bila idara kuweza kuleta BQ na inakuwa changamoto. Nakubaliana na Mheshimiwa Nyawira kwamba *pending bills* sanasana zinatokana na kukosa mipango ambayo inazingatia bajeti. Kwa mfano katika wadi kama kuna barabara inatengenezwa kwa mfano *AP line* ama *Ruai Road* utapata zimetengewa pesa lakini hakuna BQ.

Wanapokuja kutengeneza utakuta hiyo barabara imechukua pesa nyingi kuliko zile ambazo tulikuwa tumeweka kwa bajeti na hapo ndipo matatizo yanaingilia. Hii kamati ambayo

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mimi ni naibu mwenyekiti tutakuwa mstari wa mbele kuhakikisha haya mambo yametekelezwa. Kwa mfano najua huu mwaka lazima tutakuwa na changamoto. Tunaelekea kupita robo ya kwanza na kwa sasa hakuna hata BQ moja imetolewa. Hii ni kumaanisha tukifikia mwezi wa tano mwaka ujao tutakuwa na shida.

Utakuta mwezi wa tano na mwezi wa nne ndio tunapatiana kandarasi za hizo barabara ili wazifanyie kazi ilhali tulikuwa na wakati mwingi na maofisa ambao wanafaa kufanya hivyo wamezembea kwa kazi. Nimekuwa mstari wa mbele nikisema kila mwaka kabla ya kufanya bajeti tuwe na BQ za hizo barabara. Niliingia katika hiyo idara na nikawachukua wahandisi na tukaenda nao lakini hadi wa leo hakuna BQ imetoka na najua wameonyeshwa barabara nyingi.

Bwana Spika ni lazima sisi wote tuungane na tushikane. Umoja ni nguvu kwa hivyo tuweze kutembea na hii serikali na tufuate hao maofisa mpaka tuhakikishe kazi imetendeka kulingana na vile inastahili. Bwana Spika, yangu ni hayo na kamati iliweza kutoa mapendekezo yao na hiyo ni moja ya zile ambazo nimesema. Nafikiri Waheshimiwa ambao wako katika Bunge hili wataweza kukubaliana na hii ripoti kwa sababu hii ni ripoti ambayo inaeleza vile pesa zimetumika.

Kwa sababu Mheshimiwa Mutahi yuko hapa atasimama ili atetee Matanya na Chuma na Solio ili waweze kupata hizi pesa. Tukifanya hivyo tutakuwa tunawasaidia wananchi ambao walituleta hapa. Asante sana, Mungu awabariki na naomba hii ripoti iungwe mkono.

Speaker: What is it Hon. Mutahi?

Hon. Mutahi Muritu: Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Speaker: What is it?

Hon. Mutahi Muritu: Natoa mchango.

Speaker: We have not yet proposed the question. Just wait for the debate.

Hon. Mutahi Muritu: Nilikuwa nimetoka kidogo Mheshimiwa Spika.

Speaker: Okay, kindly be seated.

(Question proposed)

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, nasimama kutoa mchango na pili nikiri kama kuna idara ambayo imefanya kazi vizuri sana katika hii Kaunti na nikiulizwa niweze kupeana alama nitapatia hii idara. Kama hizi fedha zinajadiliwa hapa kama vile RMLF iko na utaratibu wake. Hizi fedha huwa zinatoka kwenye wizara. Tayari hata naibu wa mwenyekiti analegalega kwa sababu sasa hivi tunavyoongea tulipopitisha bajeti, utaratibu wa huo mfuko barabara tayari zimetumwa.

Barabara ambazo zinakusudiwa kujengwa na hiyo ruzuku zimepokelewa. Zimewasilishwa kwenye wizara husika na zinajulikana ni barabara zipi. Pili, kusema ukweli tumekuwa tukiongelea wizara yenyewe. Tumekuwa tukiongea kuhusu idara zetu. Idara ya Ardhi na Miundo mbinu katika Kaunti ya Laikipia ni pana kwa sababu huko kuna idara ya nyumba na mipango. Nilishtuka wakati kulikuwa na mkurupushane hapa.

Wengine waliona ni kama napendekeza tukiwa katika kamati fulani kugawa hilo kwa sababu ya kugawa majukumu. Ilionekana labda ni vyeo tunataka lakini mahali nimefika nimebakisha miezi tisa na sina shinikizo lolote. Niko na starehe kwa sababu nisipopata hapa Mwenyezi Mungu atanisaidia mahali pengine. Hata naibu wa Mwenyekiti atakapokuwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

anajadili ukisoma hii ni kamati ya *Transport and Public Works*. Wamesahau *Planning and Housing* iko kwenye hiyo idara.

Gavana mwenyewe alichukua hatua zaidi ya kuweza kupatia maofisa watendaji wawili katika hiyo idara. Alifanya hivyo ili kuweza kugawanya majukumu. Pia wapimaji wako kwenye hiyo idara. Mheshimiwa kutoka Thingithu aliposema amewahi kuwachukua wahandisi na kuwapeleka katika maeneo yake ili kukagua barabara akubali wahandisi ni wachache katika hiyo idara...

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Mheshimiwa Spika. Nilikuwa nataka kumfahamisha Mheshimiwa kutoka Tigithi.

Speaker: Mheshimiwa Mutahi unahitaji kufahamishwa?

Hon. Mutahi Muritu: Anifahamishe zaidi ili tuweze kuelezana kabisa.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika, ningeteka kumuelezea ya kwamba mambo ya kupanga na ujenzi iko katika kazi za umma na wakati tumesema kazi za umma, hiyo yote iko hapo ndani. Ni mambo mengi lakini ni vile tu hatuwezi elezea kila kitu kinafanyika hadi *surveying.* Kazi za umma ni mwavuli ya zile zingine zote ambazo ziko hapo chini.

Hon. Mutahi Muritu: Asante. Wacha tusibishane sana. Mheshimiwa Spika, umenifurahisha sana kwa sababu umechukua kanuni zetu kuweza kuangalia ili uone hayo majukumu. Hata kama unasema Uchukuzi na kazi za Umma pia huwa katika idara zote. Kuna Idara ya Kazi za Umma kwa afya na kwa hivyo ninapojaribu kuelezea kile nilichokuwa nasema, hata hili Bunge tutakapotoka, aidha tuwe tutarudi au hatutarudi, jukumu tulilopewa ni kuweka mambo sawa.

Nimekiri hapa nikasema ya kwamba Gavana mwenyewe ameweza kugawanisha hiyo idara na akaleta maafisa wawili hapa. Kuna ofisa ambaye anasimamia mambo ya miundo mbinu na mwingine anasimamia mipango na manyumba katika hii serikali. Tuliwapitisha hapa kwenye hili Bunge na kwa hivyo hata sisi tunapofanya hivyo, ningetaka akiri hapa na aweze kunipa changamoto kidogo.

Tuko na wahandisi pale na kuna mmoja ambaye mimi namjua ambaye anaitwa Kairu. Yule msichana anayefanya naye pale wako na kazi nyingi sana. Kwa hivyo katika hiyo idara yenyewe tunaposema labda hawajawajibika ilivyo kwa sababu uwezo katika hiyo idara ni kidogo sana. Hebu fikiria, tuko tu na mhandisi mmoja hapa na mwingine Nyahururu. Kama Laikipia Magharibi ni pana na kuna mhandisi mmoja tu. Ukija hapa nafikiri Kairu ndiye mhandisi wa pekee hapa na nafikiri ndiye tu ambaye anayesimamia Laikipia Kaskazini.

Kwa hivyo tunapoangalia kutokuwa na wajibikaji na kuharakisha kuuliza ni kwa nini hizi BQ zimechelewa, ukienda pale ni ofisi moja. Hata tunapoandika hii ripoti na wanapotoa haya maono, nguvu na kazi pale inahitajika kuwawezesha wale maofisa ili kazi ifanyike. Kama sasa hivi tumepitisha bodi na yule mhandisi ndiye anayeenda kwenye hizo miji zote zilizolengwa kufanya kazi. Kwa hivyo hii idara ninaitetea 100% kwa sababu ninaamini ya kwamba awe ni yule ofisa ambaye aliondoka anayeitwa Karanja au mwingine aliyeingia Bwana Mwangi, anafanya kazi kwa kujitolea sana.

Kama kuna watu ambao hujitolea, mgala muue na haki umpe, zaidi ni hiyo idara. Hiyo idara huwa wanafanya kazi ilivyo. Mimi sipingani na ripoti lakini tunapoangalia mahesabu, pia tuangalie uwezo wa nguvu kazi, na wataalamu walioko kule. Ni cha umuhimu zaidi kwa sababu hizi fedha zinazotoka, kama sasa hivi nimesema ya kwamba hizo pesa mipango imewasilishwa na kunajulikana ni barabara zipi zitakapojengwa. Ninaona Mheshimiwa kutoka Thingithu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

amesema ya kwamba hiki ni kipindi kilichomalizika Desemba 2019 na kwa hivyo inaonekana ya kwamba 2021 itakuja kujadiliwa na Bunge lijalo. Itakuwa ni muhimu na kwa hayo mengi au amchache, ninaunga mkono. Asante.

Speaker: Thank you, Hon. Mutahi. Just to make a clarification, the motion talks of the Transport and Public Works Committee and I think that is the correct name as far as our Standing Order is concerned in the 1st Schedule until when we will have amended the Standing Orders. Housing, Mapping and Planning is under the Committee of Finance and County Planning. Therefore, that is not under the oversight of Transport and Public Works. I think we need to get that clarification well. So that is the clarification I needed to make. It is now time for the mover to give a reply.

Hon. Catherine Nyawira: First I want to thank the Hon. Members for their contribution towards this report. Secondly, in seconding the report, the vice chair was saying that this department has got laxity. I don't know what he meant by that but I believe that we were going through this report together and we were clear on what MRF has done. We saw the improvements on our roads on parking spaces which have been created in Laikipia County and therefore it means that the department is collecting more on parking fees.

It means that it is collecting more on hefty fines which are placed when people do not pay parking fees or park their cars on wrong places and also obstructions. When we were looking at the report we noted that this is where that extra money is coming from and I think he is the same one who asked that question in the committee. I don't know whether the Nanyuki Hospital is in Thingithu or Nanyuki but there are people who are chased from the road to create parking fees and that is where this, money has come from. It was just a clarification. I urge the Members to pass this motion.

Speaker: Hon. Members, the question for that motion will be put on Tuesday, 7th September, 2021 at 2.30 p.m.

ADJOURNMENT

Speaker: This House now stands adjourned until next week on Tuesday, 7th September, 2021 at 2.30 p.m.

The House rose at 3.28 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*